

Wapo wanatofautisha maneno haya mawili, na wapo wanayoyaona kama ni kitu kimoja..

Ni kweli Bwana Yesu alituonyesha kuwa “maandiko na Neno” la Mungu ni kitu kilekile kimoja, na ndivyo ilivyo..

Soma Yohana 10:35

*Ikiwa aliwaita miungu wale waliojiliwa na neno la Mungu; (na maandiko hayawezi kutanguka);*

Isipokuwa tofauti yao ndogo ni kwamba maandiko yanajifunga tu katika maandishi.. lakini Neno la Mungu, ni aidha katika maandishi au kuzungumzwa.

Bwana anaweza kutoa ujumbe wake kwa sauti kinabii, vilevile anaweza kuzungumza kwa biblia (maandiko). Na zote zikawa sauti zake zenye majibu.

Lakini tulichopewa, na tunapaswa tukitegemee sana ni Neno la Mungu katika maandiko, alisema, “maandiko hayawezi kutanguka”, yaani

kilichoandikwa kimeandikwa. Lakini Neno lake katika sauti anaweza kulitangua mwenyewe, au akaghahiri, au likawa la muda tu, tofauti na Neno katika maandishi.

Hivyo ukiishi kwa hilo, utakuwa salama. Lakini tukiwa wavivu wa kujifunza biblia. Tuwe na uhakika kuwa tunapoteza maisha yetu.

Marko 12:24

*[24]Yesu akajibu, akawaambia, Je! Hampotei kwa sababu hii, kwa kuwa hamyajui maandiko wala uweza wa Mungu?*

Tupende Biblia zaidi ya chakula, tuone kuwa hatuwezi kuishi bila hilo; Daudi alisema.

Zaburi 119:140

*[140]Neno lako limesafika sana, Kwa hiyo mtumishi wako amelipenda.*

Tofauti kati ya maandiko na Neno ni ipi?

Tuyapende maandiko, kwani ndio uhai wetu.

Bwana akubariki.

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

**Mada Nyinginezo:**

**Gombo ni nini?**

**Chuo cha vita vya Bwana ni kipi?(Hesabu 21:14)**

**Kitabu cha YASHARI kinachozungumziwa katika 2Samweli  
1:17-18, ni kitabu gani?**

**Tofauti kati ya mtu na mwanadamu ni ipi?**

**Nini maana ya “Torati na manabii”?**

Tofauti kati ya maandiko na Neno ni ipi?

**Yeshuruni ni nani katika biblia?**

**URIMU NA THUMIMU NI NINI KATIKA BIBLIA?**

**Rudi nyumbani**

Share on:  
WhatsApp